ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*SUPPLEMENT NO. 36* **4th September, 2020**

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No.36. Vol.. 36 Dated 4th September, 2020*
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na 740 La Tarehe 4/9/2020

SHERIA YA BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA
(SURA YA 49)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 28)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA USAJILI WA VYAMA VYA MICHEZO ZA MWAKA 2020

Jina la Kanuni Tangazo Na. 442 la mwaka 1999

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Usajili wa Vyama vya Michezo za Mwaka 2020 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Usajili wa Vyama vya Michezo za mwaka 1999 ambazo zitajulikana kama "Kanuni Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 19

2. Kanuni Kuu zinarekebisha kwenye kanuni ya 19 kwa -

(a) kufuta kanuni ndogo (1) na badala yake itasomeka kama ifutavyo:

“(1) Wakuzaji wa michezo (promoters), wakala (agents) au taasisi nyingine yoyote inayojishughulisha na michezo watatakiwa kusajiliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi ili kuendesha shughuli zao na watatakiwa kupata vibali kutoka Baraza au Kamati za Michezo za ngazi husika.”;

(b) kuondoa maneno "kanuni zilizopo" yaliyo mwisho mwa kanuni ndogo (2) na kuweka maneno "kanuni hizi";

(c) kufuta kanuni ndogo ya (3) na badala yake kuweka kanuni ndogo mpya zifuatayo:

"(3) Wakuzaji, wakala au taasisi yoyote inayojishughulisha na mchezo wowote haitapewa kibali cha kuendesha shughuli zozote za michezo pasipo kusajiliwa na Baraza.

(4) Klabu, chama au shirikisho lolote la michezo halitapewa kibali cha kuendesha shughuli yoyote ya michezo ambayo inashirikisha wakuzaji, wakala au taasisi yoyote ambayo haijasajiliwa na Baraza.

(5) Kwa ajili ya matumizi ya kanuni hii, 'taasisi' inamaanisha -

(a) asasi yoyote binafsi au ya Serikali;

(b) shule yoyote ya michezo (sports academy), isipokuwa kama shule au taasisi husika ilianzishwa kwa sheria ya Bunge iliyoipa mamlaka hayo;

(c) kituo cha michezo (sports centres);

(d) kituo cha kufanyia mazoezi ya mwili (fitness/ gym centres); au

(e) taasisi nyingine yoyote itakayojihusisha na mafunzo au mazoezi ya mwili kupitia michezo."

Marekebisho ya kanuni ya 24

11. Kanuni Kuu zinarekebisha kwenye kanuni ya 24 kwa kuondoa maneno 'kama ifuatavyo' yaliyo mwisho wa kanuni hiyo, na badala yake kuweka maneno "kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza".

Marekebisho ya kanuni ya 25

12. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 25 na badala yake isomeke kama ifuatavyo:

"Kuwasilisha maombi kwa Baraza kwa ajili ya kulipa tozo

25. Mtu, chama, shirikisho au asasi yoyote inayotaka kusoma rejista ya usajili, kukagua jalada la chama chochote cha michezo, kupata kivuli cha cheti, hati iliyothibitishwa na Baraza, kuwasilisha

mabadiliko ya viongozi au kupatiwa nakala ya hati yoyote iliyo katika hifadhi ya Baraza kwa ajili ya matumizi yake halali, atapaswa kuwasilisha maombi ya maandishi kwa Baraza na kulipa tozo zilizoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.".

Nyongeza ya kanuni ya 26

13. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kanuni ya 25 kanuni ifuatayo:

"Adhabu kwa kushindwa kulipa ada za usajili

26. Klabu, chama au shirikisho la michezo litakaloshindwa kulipa ada za usajili kwa mujibu wa Kanuni hizi kitachukuliwa hatua zifuatazo:

(a) kutoa onyo la maandishi kwa watakaochelewa kulipa ada za mwaka kwa siku zisizozidi 30;

(b) kutoza faini ya asilimia tano (5%) ya kiasi cha ada ambacho hakijalipwa kwa kila mwezi baada ya siku ya 30 tangu ada hiyo ilipopaswa kulipwa;

(c) kusitisha usajili wa chama ambacho hakijalipa ada husika kwa zaidi ya siku 90 ili kukizuia kujishughulisha na masuala ya michezo hadi watakapolipa ada husika; na

(d) kufuta usajili wa chama husika katika rejista ya michezo endapo ada husika haijalipwa katika kipindi cha zaidi ya siku 90 tangu kusitishiwa shughuli zake. ".

Marekebisho ya kanuni ya 27

14. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kubadili kanuni ya "26" ya awali na kuwa kanuni ya "27".

Nyongeza ya Jedwali

15. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kuongeza Jedwali jipya lifuatalo:

" JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 24)*

ADA MBALIMBALI

| NA | AINA YA CHAMA | KIWANGO | |
|---|---|---|---|
| | | ADA YA USAJILI (Itatolewa mara moja wakati wa usajili tu) | ADA YA MWAKA (itatolewa kila mwaka) |
| 1. | Vyama vya Michezo vya Kitaifa vyenye wanachama wa Mikoa | 200,000/= | 150,000/= |
| 2. | Vyama vya Michezo vya Kitaifa Vingine | 200,000/= | 100,000/= |
| 3. | Vyama vya Michezo vya Mikoa | 100,000/= | 50,000/= |
| 4. | Vyama vya Michezo vya Wilaya | 100,000/= | 50,000/= |
| 5. | Vyama vya Michezo ambavyo ni Taasisi (Taasisi za Michezo) | 100,000/= | 100,000/= |
| 6. | Vilabu vinavyoshiriki mashindano ya Vyama vya Kitaifa | 100,000/= | 100,000/= |
| 7. | Vilabu vinavyoshiriki mashindano ya Vyama vya Mikoa na Wilaya | 100,000/= | 50,000/= |
| 8. | Wakuzaji na Wakala wa Michezo | 200,000/= | 100,000/= |
| 9. | Shule za Michezo (Sports Academies) | 100,000/= | 100,000/= |
| 10. | Vituo vya Michezo (Sports Centres) | 100,000/= | 100,000/= |
| 11. | Vituo vya Mazoezi ya viungo (GYM &Fitness Centres) vya Kisasa | 100,000/= | 150,000/= |
| 12. | Vituo vya Mazoezi ya viungo (GYM &Fitness Centres) vya kawaida | 100,000/= | 100,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 25)*

TOZO NYINGINEZO

| NA. | AINA YA MAOMBI | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya kusoma rejista (perusal fee) | 50,000/= |
| 2. | Maombi ya kupatiwa hati iliyodhibitishwa na Msajili au kuidhinisha hati inayoletwa na mdau. | 50,000/= |
| 3. | Maombi ya kivuli cha cheti au hati nyingine iliyo katika hifadhi ya Baraza | 50,000/= |
| 4. | Kuwasilisha marekebisho ya katiba kwa Msajili | 50,000/= |
| 5 | Kuwasilisha mabadiliko ya viongozi wa klabu,chama au shirikisho cha michezo pale ambapo viongozi wamebadilika kwa sababu nyingine bila kubadili umiliki | 10,000/= |
| 6. | Kuwasilisha mabadiliko ya umiliki wa klabu cha michezo pale ambapo klabu kimeuzwa kwa mtu au taasisi nyingine | 2% ya mapato ghafi la mauziano |
| 7 | Maombi mengineyo | 50,000/= |

”

Dodoma,
25 Agosti, 2020

HARRISON G. MWAKYEMBE
*Waziri wa Habari, Utamaduni,*
*Sanaa na Michezo*